KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

# Al-Hudaa [Uongofu]

# الهدى

25/= Ksh

Volume 9, Issue 1

27th Rabee ul-Aakhar 1432

1st April, 2011

## MIONGONI MWA MAADUI WAOVU KABISA ULIMWENGUNI

Mtayarishi: Sheikh Jamaal Ibn Furayhaan al-Haarithee

### MBWA WA MOTONI

Imepokewa kutoka kwa Abee Awfee (رضي الله عنه)yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Ma-Khawaarij ni mbwa wa motoni." [Ibnu Majah: 173 / Ahmad: 4/355 na imetangazwa kuwa na daraja ya Hasan na Shaykh Al-Albaanee.] Imepokewa kutoka kwa Abu Umaamah yakwamba amesema: "Watu waovu zaidi waliowahi kuchinjwa chini ya mbingu/ juu ya uso wa ardhi, na wale ambao wao waliowahi kuwachinja ndiwo waliokuwa miongoni mwa watu bora, mbwa wa motoni. Mwanzoni wao walikuwa ni Waislamu lakini wakakufuru." Mimi nikasema: "Ewe Abu Umaamah! Wewe utasemaje maneno kama hayo?" Akasema: "Bali mimi niliyasikiya kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) [Ibnu Maajah: 176. Imepewa daraja ya Hasan na Shaykh Al-Albaanee.

### Ma-Khawaarij Wamuuwa 'Alee (رضي الله عنه)

Amepokea Imaam at-Twabaraani katika Kitabu chake "at-Tareekh" [3/156] kutoka kwa Ismaa'eel ibn Raashid yakwamba alisema: "Kutoka kwenye kumbukumbu zinazohusiana na Ibn Muljim na wenzake ambao ni ma-Khawaarij, ni kwamba yeye, Al Baraak ibn 'Abdillaah na 'Amru ibn Bakr At-Tameemee – ambao ni miongoni mwa viongozi wa ma-Khawaarij – walikutana ili kuyajadili mas'ala yanayowahusu watu. Wakawakashifu viongozi na kisha wakawataja ma-Khawaarij wa Nahrawaan [Hawa ni ma-Khawaarij waliopigana na 'Alee (رضي الله عنه) katika vita vya Nahrawaan], wakawaombea Baraka ziwashukie wao, kisha wakasema: "Sasa sisi tufanyeje baada ya kufa kwao, kwa hakika wao walikuwa ni ndugu zetu, ambao waliokuwa ni wenye kuwalingania watu kwenye kumuabudu Mola wao bila ya kujali (au kuogopa) lawama za wenye kulaumu katika [dini ya] Allaah. Lau kama sisi tungelikuwa ni wenye kujitolea maisha yetu na tukawakabili ma-Imaam wa upotofu na tukajaribu kuwauwa kwa sababu ya kuzikomboa sehemu za ardhi kutoka kwao na kulipa visasi vya ndugu zetu."

Kadhaalika ndivyo yalivyokuwa mikao ya siri ya ma-Khawaarij.

Akasema Ibn Muljim: "Mimi nitawaondolea dhiki muliyonayo ya 'Alee Ibn Abee Twaalib!" Nae alikuwa (Ibn Muljim) ni miongoni mwa watu wa Misr (Egypt)." Al-Baraak ibn 'Abdillaah nae akasema: "Mimi nitawaondolea dhiki muliyonayo ya Mu'aawiyah ibn Abee Sufyaan!" Akasema 'Umar ibn al-Bakr: "Mimi nitawaondolea dhiki muliyonayo ya 'Amr ibn Al 'Aass!" Kisha baada ya hapo, wakala viapo kwa jina la Allaah yakwamba hapana miongoni mwao atakaemkosa aliyemlenga mpaka emma amuuwe au auwawe yeye. Wakayachukuwa mapanga yao wakayapaka sumu, wakajiandaa vilivyo na wakala viapo katika siku ya kumi na saba ya mwezi Mtukufu wa Ramadhaan."

Kadhaalika ndivyo yalivyokuwa mikao ya siri ya ma-Khawaarij, hupanga njama za kuwauwa Waislamu.

Amma kumuhusu huyu Ibn Muljim al-Maraadee, alisafiri na kukutana na marafiki zake katika mji wa al-Koofah na akawa ameihifadhi kwenye siri yake niya yake ili wasijue kuhusu ujumbe alokuja nao. Hapo alikutana na msichana mmoja aliyekuwa mrembo kutoka katika kabila la Tameem ar-Rabaab aitwae Qataam Bint ash-Shajinah. Bakake pamoja na ndugu yake waliuwawa kwenye vita vya Nahrawaan. Alipomuona msichana huyo, alichanganyikiwa mpaka akausahau ujumbe alokuja kuutekeleza na akafunga nae ndoa. Akasema (yule msichana kumwambia Ibn Muljim): "Mimi sitokubali kuolewa na wewe mpaka uniondolee sikitiko langu." (Ibn Muljim akamjibu): "Ni jambo gani hilo litakalokukuondolea wewe sikitiko lako?" Akasema (yule msichana): "Ni kumuuwa 'Alee Ibn Abee Twaalib." Akasema (Ibn Muljim): "Ama kuhusu kumuuwa 'Alee, basi mimi sijui ni kwanini wewe umemtaja yeye ikiwa mapenzi yako ni mimi." Akajibu (yule msichana): "Naam [nitakwambia ni

Yaliyomo

Miongoni mwa maadui w ... 1 - 2
Njia za kupata Msamaha... 4-2-3

# MIONGONI MWA MAADUI WAOVU KABISA ULIMWENGUNI

kwanini], jichagulie wakati ambao atakapokuwa amepumzika, ukifaulu kwa hilo basi utakuwa umenipandisha mimi daraja pamoja na wewe mwenyewe na kuishi na mimi itakuwa ni jambo lenye kupendeza. Na iwapo utauwawa, basi alilokuwekea Allaah [kwenye hazina yake] ni bora kuliko ulimwengu mzima na uzuri wake na uzuri wa watu wake." Akasema (Ibn Muljim): "Wallaahi, hakuna lililonileta mimi katika mji huu isipokuwa ni kumuuwa 'Alee, kwahivyo utapata ulililoliomba." Kisha Ibn Muljim akamfuata mtu mmoja kutoka katika kabila la Ashja' aitwae Shabeeb Ibn Najrah akamwambia: "Wewe unataka kujipatia heshima kubwa katika Ulimwengu huu na kesho Akhera?" Akajibu (Shabeeb): "Na ni heshima gani hiyo?" Akamjibu (Ibn Muljim): "Ni kumuuwa 'Alee Ibn Abee Twaalib." Akasema (Shabeeb): "Thakalatkah Ummuk! [Huu ni msemo wa kiarabu wa kukanusha kimsingi, wenye maana ya jambo lililoje la kushangaza ulolisema au ulolifanya: Maana yake ya dhahiri ni 'Mamako amekukosa']. Kwa hakika umekuja na mas'ala ya kutisha mno! Utafanya vipi kuwa na uwezo wa [kumuuuwa] 'Alee?" Akamjibu Ibn Muljim: "Tutamvizia kwenye maficho, tukimungoja aondoke kuelekea msikitini kwa swala ya asubuhi (Fajr), kisha sote tumshambulie kwa pamoja mpaka tumuuwe. Tutakapofaulu basi tutakuwa tumepata hadhi kubwa na pia tutakuwa tumejilipa kisasi chetu, na iwapo tutauwawa, basi Aliyotuandalia nayo Allaah ni bora kuliko Ulimwengu mzima na kila kilichomo ndani yake."

Na kadhaalika ndivyo walivyo ma-Khawaarij katika zama zetu hizi pamoja na mauwaji yao ya kujilipua kwa mabomu, ni kufanana kulioje kwa zama zetu na zama zilizotangulia.

Shabeeb akasema: "Ole wako! Lau angelikuwa ni yoyote asiyekuwa 'Alee , hilo lingelikuwa ni sahali kwangu mimi. Mimi nimeushuhudia ushujaa wake na ujasiri wake katika Uislamu na mkuruba wake na Mtume (صلى الله عليه وسلم) Mimi sijioni nafsi yangu kuwa na moyo mtulivu/ wenye kustarehe kuhusu kumuuwa yeye." Akasema (Ibn Muljim): "Kwani wewe hujui yakwamba yeye aliwauwa watu wa Nahrawaan, waja wema [wa Allaah], Allaahu Akbar, ni shubhah (kutoeleweka ) iliyoje hii?" Akajibu (Shabeeb): "Ni kweli hayo." Akasema (Ibn Muljim): "Basi na tumuuweni sisi kwa sababu ya wale aliowauwa katika ndugu zetu." Basi hapo Shabeeb akakubali. Wakamwendea Qataam alipokuwa kwenye 'Itiqaaf katika msikiti mkubwa na wakamwambia: "Sisi sote kwa umoja tumekubaliana kumuuwa 'Alee."

Hawa ndiwo ma-Khawaarij. Wao humuabudu [Allaah] pasi na 'Ilmu wala uongofu, na zaidi ni kwamba wao ni watu wa kufuata hawaa (za nafsi zao)." Wakachukuwa panga zao na kushika zamu ya mashambulizi nje ya mlango wa kutokea anaoutumia 'Alee. Alipotoka, Shabeeb akamvamia na upanga wake lakini ukalenga sehemu ya mlango au dirisha. Ibn Muljim - Shaqee (mwenye dhiki) – pia alimshambulia kwa upanga wake, kwenye bapa lake la uso." Mwisho wa nukuu. 'Alee (رضي الله عنه) akaaga dunia baada ya siku mbili kutokana na mashambulizi hayo. Aliyemuuwa alikuwa ni 'Abdur Rahmaan ibn 'Amru ibn Muljim Al Maraadee. Ma-Khawaarij hawakuwa na majuto yoyote juu ya kitendo chao hicho kiovu, bali wanajivunia kwa kutekeleza tendo hilo ovu na kuwaenzi waliotekeleza, wanaamini yakwamba hayo ni miongoni mwa mambo yenye kuwakurubisha kwa Allaah.

## NENO LA BUSARA

**Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم)**

**"HAKIKA MALIPO MAKUBWA HUTOKAMANA NA MAONDO MAKUBWA [MITIHANI]; NA HAKIKA ALLAAH ( سبحانه وتعالى) PINDI ANAPOWAPENDA WATU, HUWALETEA MITIHANI, WENYE KUYARIDHIYA HAYO WATAPATA RADHI ZAKE NA WENYE KUYACHUKIYA WATAKHASIRIKA."**

**Imaam at-Tirmidhee**

*(Endelea kutoka Ukurasa wa 4)*

**NJIA ZA KUEPUKA ADHABU:**

Ndugu mpendwa, Ibn Taymiyyah ( رحمه الله) alisema kuwa muumin huenda akajilinda na adhabu ya dhambi alilolfanya kumuangukia kwa njia kumi zifuatazo

1. Kutubia kwa Allaah toba ya kikweli kweli ili Allaah amsamehe, kwa sababu yule anaye tubu kweli kutokana na madhambi nikama yule ambaye hakufanya
2. Kuomba msamaha kwa Allaah ili Allaah amsamehe
3. Kufanya yalo mema ambayo yatafuta madhambi. Allaah asema "**Nasimamisha swala katika ncha mbili za mchana (Adhuhuri &Asr). Na swala (wakati wa usiku) zilizo karibu na mchana (Maghrib & Ishai). Hapana shaka mema huondosha mabaya ; hayo ni mawaidha kwa wenye kuwaidhika."(Hood:114).**
4. Ndugu zake katika imani wamuombe msamaha.
5. Baadhi ya ndugu zake katika iman watoe ajra ya mema yao yamfikie yeye.
6. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amshufaie (amuombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu) ili Allaah asimuadhibu
7. Allaah ampe mitihani katika maisha, ikiwa ni mali, hali, watoto au familia
8. Allaah kumtia kwenye mitihani ndani ya kaburi.
9. Allaah kumtia kwenye mitihani na vitisho vya siku ya kufufuliwa
10. Allaah kumsamehe kutokana na Rehma yake

Yeyote atakaye kosa njia hizi kumi zote atakuwa hana wakumlaumu ila nafsi yake. Allaah asema kwenye hadithi Qudsi "Bali hayo ni matendo

*(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)*

*(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)*

yako, nayaandika, kisha nakulipa inavyostahiki (kulingana na madhambi yako); Kwa hivyo ataye yaona mazuri, basi na amshukuru Allaah, nayeyote atakaye ona vingine, basi na asimlaumu mwingine ila nafsi yake.

**NJIA ZA KUEPUKA JAHANAM:** Kama vile Allaah alivyo tupatia njia za kupata msamaha na radhi zake, Yeye pia ametupa njia za kuepuka jahanam, Allaah asema "**Kila nafsi itaonja mauti na hapana shaka mtalipwa thawabu zenu siku ya Qiyamah. Na mwenye kuepushwa na moto na kutiwa peponi hakika amefuzu.Na hayakuwa maisha ya ulimwengu ila ni starehe na udanganyifu." (Aal'Imraan:185).**

**BAADHI YA NJIA HIZO NI:**

**KUSUBIRI BAADA YA KUFILIWA NA WATOTO WATATU:** Mtume (صلى الله عليه وسلم)alisema, "Allaah ameharamisha moto kwa yule ambaye amewazika watoto wake watatu huku akiwa na subra."(Tabaraani)

**KULEA MABINTI WATATU, AU MADADA, KWA USAWA NA KUWA MWEMA KWAO: '**Aaisha (رضي الله عنها) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Hakuna katika ummah wangu yeyote, atakaye walea mabinti watatu au madada na akawa mwema kwao, basi watakuwa kama ngao kwake na moto." (Bayhaqi).

**KUMUHAMI NA KUMNUSURU MU'MIN ASIPOKUWEKO:** Asmaa' (رضي الله عنها) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema yoyote ataye mtetea ndugu yake akiwa hayupo dhidi ya watu wanao msegenya, Allaah atamuacha huru na moto." (Ahmad).

**KUSWALI SIKU ARUBAINI KWA JAMAA'AH NA KUHUDHURIA TAKBEER YA KWANZA:** Anas (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Yeyote ataye swali siku arubaini na akahudhuria takbeer ya kwanza basi atakuwa huru na unafiki na moto wa Jahanam." (at-Tirmidhee).

**TABIA NJEMA:** Abu Hurayrah (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Allaah ataharamisha moto wa Jahanam hata kumgusa yule ambaye anatabia njema mpole." (Al-Haakim).

**KUSWALI FAJR NA 'ASR (KWA JAMAA'AH):** 'Umaarah ibn Ruwaybah (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Atakaye swali Fajr na Asr, hatoingia motoni." (Muslim).

**NJIA ZA KUSTAHIKI KUPATA PEPO:** Kutamka shahada mbili *[LA ILAHA ILA ALLAAH WAANA MUHAMMADAN RASULLAH]* na kutekeleza. 'Ubaadah ibn As-saamit (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Allaah atamtia peponi mbali na amali zake, yeyote atemkae, 'nashuhudia( kwa kutemka kwa ulimi na kukiri kwa moyo) kuwa hapa mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah na Muhammad ni mtumwa wake na mjumbe wake na 'Eesaa ni mtumwa wake na mjumbe wake na Neno lake alilo liweka kwa Maryam na Ruh.' Na kuwa Pepo ni haki na Jahanam ni haki." (Al-Bukhari &Muslim).

**KUYAHIFADHI MAJINA MAZURI YA ALLAAH:** Abu Hurayrah (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema. "Allaah ana majina tisiini na tisa, yeyote atakae yahifadhi ataingia peponi." (kuyahifadhi yamaanisha kuyahifadhi, kuyaamini, na kuyatendea kazi kulingana nayo.

**KUSOMA AYAT AL– QURSIYY BAADA YA KILA SWALA YA WAJIB:** Abu Umaamah (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Hakuna kinacho mzuia yule anaesoma ayat Al-Kursi kila baada ya swala ya wajib kuingia peponi ila kuwa yeye bado yuko hai." (An-Nasaa'i).

**KUTOA SWADAKA.** Huthayfah (رضي الله عنه ) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Yoyote atakaye toa sadaqa kwa ajili ya Allaah , na akafa akifanya hivyo ataingizwa peponi." (Ahmad).

**KUMSAIDIA YATIMA KWA MALI:** Sahl ibn Sa'd (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Nitakuwa karibu hivi na yule atakaye mpa msaada yatima (kisha akashikanisha kidole chake cha katikati na cha tashahud)."

**KUHIFADHI ULIMI NA SEHEMU ZA SIRI:** Sahl ibn Sa'd (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Yeyote atakaye hifadhi ulimi wake na sehemu zake za siri, nitamhakikishia pepo." (Al-Bukhari).

**MKE KUMTWI'I MUMEWE:** Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema , " Ikiwa mwanamke ataswali swala zake tano, akafunga ramadhan, akahifadhi sehemu zake za siri, na akamtii mumewe, ataingia peponi mlango autakaye yeye." (Ibn Hibban).

**KUWA MBALI NA KIBURI, DENI NA WIZI WA NGAWIRA:** Thawbaan (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Yoyote atakaye kufa na akawa mbali na kiburi, na deni na kuiba ngawira ataingia peponi." (at-Tirmidhee).

**KUWA MTAWALA MUADILIFU, MKARIMU NA ASIWE MZINIFU:** 'Iyaadh ibn Himaar (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Watu sampuli tatu nikatika watu wapeponi mtawala muadilifu ambaye atumia vyema mali yalio chini ya ulinzi wake, mtu mwenye moyo wa wema kwa ahli zake (family) na waislamu kwa jumla, na mtu muhitaji mweye familia asie uliza watu kumsaidia.

**KUONDOSHA VITU VYENYE KUDHURU NJIANI:** Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Nilimuona mtu akistarehe peponi kwa sababu aliukata mti ambao ulikuwa ukiwadhuru watu uliokuwa katikati ya njia." (Muslim).

Kumuegezea mtu mda wakulipa deni asiloweza kulilipa. Huthayfah (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (s.aw) alisema, " Mtu alikufa akaingia peponi, akaulizwa, 'Nikitu gani ulichokifanya kikakuingiza peponi? 'akjibu, 'Nilikuwa nikifanya biashara nakiwapa mda waziada wale wasioweza kunilipa nakuwafanyia...

[**ENDELEA KATIKA JARIDA LIJALO**]

# NJIA ZA KUPATA MSAMAHA (MAGHFIRAH) Imaam Ibn Taymiyyah

Namshukuru Allaah, Mwenye kusamehe madhambi, Mwenye kukubali Toba. Na swala na salamu zimfikie Mtume (صلى الله عليه وسلم) na ahli zake na maswahaba wake na wenye kuwaandama kwa wema mpaka siku ya Kiyama. Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Sema: Enyi waja wangu waliokiuka mipaka katika kufanya ma'asiya, musikate tamaa na Rehma za Allaah. Hapana shaka Allaah huyasamehe madhambi yote. Hapana shaka Yeye ni Mwingi wa msamaha (Raheem)."** [az-Zumar: 53]

Vilevile amesema, **"Na simamisha swala katika ncha mbili za mchana (adhuhuri na al-'Asri). Na swala (wakati wa usiku) zilizo karibu8 na mchana (Magharibi na Ishaa'). Hapana shaka mema huondosha mabaya, hayo ni mawaidha kwa mwenye kuwaidhika."** [Hud: 11]

Msomaji mpendwa, sote twakosea na sote twahitaji mno msamaha kwa madhambi yetu tuyatendao mchana na usiku. Ni kwa ajili ya Huruma ya Allaah juu yetu, akatuwekea njia nyingi zaq kupata msamaha. Muislamu atakaposhikamana na njia hizo, isipokuwa ataingizwa katika Maghfira na Rehma za Allaah. Akidumu kwenye Imani na asimshirikishe Allaah, kwa sababu ushirikina na ukafiri wazuiya kupatikana kwa Maghfira. Allaah amesema: **"Hapana shaka Allaah hasamehi kushirikishwa (na kitu chochote). Na asamehe isiyokuwa shirk kwa amtakaye. Na yeyote anayemshirikisha Allaah, hakika amekwisha potea upotevu uliombali (na haki)."** [an-Nisaa' 116]

**NJIA ZA KUPATA MSAMAHA**: Hizi ni baadhi za njia ambazo Allaah amezifanya ziwe ndizo zenye kusababisha kupatikana msamaha wa madhambi, ili mtu asivunjike moyo na kukata tamaa ya Rehma ya Allaah, na ili mtu vilevile akimbilie kwenye wema, kama alivyosema Allaah, **"Na fanyeni haraka kuomba msamaha kutoka kwa Mola wenu (kwa kufanay twa'a) na pepo upana wake ni (kama upana wa) Mbingu na Ardhi iliyoandaliwa kwa wenye kumcha Allaah."** [Aali-'Imaraan: 133]

**UISLAMU:** Allaah amesema: **"Waambie waliokufuru wakiacha ukafiri watasamehewa makosa yaliotangulia. Na wakirudi (kutaka kukupiga wewe) hakika zimekwisha pita nyenendo za (kuwaangamiza) waliotangulia (waliokuwa wakiwakanusha Mitume)." (Al-Anfaal:38).** 'Amr ibn Al-'Aas (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema. "Hukujua kuwa kusilimu kwa ondosha yote yaliopita mabaya?"(Muslim).

**HIJRA:** Nayo ni kugura kutoka nchi ya ukafiri kwenda nchi ya kiislamu. Allaah amesema **"Kisha hapana shaka Mola kwa waliohama baada ya kuadhibiwa (na makafiri) kisha wakapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu na walisubiri, hapana shaka Mola wako baada ya hapo ni Mwingi wa msamaha, Mwenye huruma."(An-Nahl:110).** 'Amr ibn Al-'Aas (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Hijra yafuta mabaya yaliopita"

**HIJJAH ILIOKUBALIWA:** 'Amr ibn Al-Aas (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema. "Hajj makbool yafuta mabaya yaliopita" (Muslim). Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), alisema, "Yeyote anayefanya Hajj na asifanye mambo ya ndoa wala madhambi (wakati wa Hajj), atarudi kutoka Hajj hali kama ile aliyozaliwa na mamake (bila dhambi)." (Al-Bukhari).

**DUA WAKATI USIKIAPO ATHAAN:** Sa'd ibn Abi Waqqaas (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), alisema "Yeyote atakayesema wakati atakapo msikia muathan, 'mimi pia nashuhudia kuwa hapana Mola wakuabudiwa kwa haki ila Allaah peke yake na nashuhudilia kuwa Muhammad ni mtumwa wake na mjumbe wake. Namkubali Allaah kama Mola, na Muhammad kama Mtume, na Al-islam kama dini'-madhambi yake yote asamehewa." (Muslim).

**KUAFIKIANA NA MALAIKA WAKATI UKISEMA AMEEN:** Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Wakati Imaam akisema 'Ameen; sema 'Ameen; kwa sababu yeyote atakaeafikiana na Malaika wakisema Ameen atapata kusamehewa madhambi yake yote yaliopita." (Al-Bukhari & Muslim).

**KUAFIKIANA NA MALAIKA WASEMAPO (RABANAA WALAKAL HAMD)** Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Wakati Imaam akisema 'samia Allaahu liman hamida', sema 'Rabanaa walakal hamd', kwa sababu yeyote atakaye afikiana na malaika wakati wakisema hayo atapata kusamehewa madhambi yake yote yaliyopita." (Al-Bukhari & Muslim)

**KUSWALI RAKAA MBILI KWA MAZINGATIO:** Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema. "yeyote atakayeswali rak'aa mbili zozote bila yakutokuwa muangalifu atapata kusamehewa madhambi yake yote yaliopita," (Ahmad).

**KUKAA KWENYE MAKUNDI YANAYO MATAJA ALLAAH:** Sahl ibn Hanthalah (رضي الله عنه), alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema "Haitokuwa kundi la watu wakutana kwa ajili ya kumtaja Allaah ila wataambiwa wakati waondokapo kuwa 'Madhambi yenu yamesamehewa.'" (Ahmad).

**MARADHI:** Aa'ishah (رضي الله عنها), , alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema. "Popote auguapo Muumin atatakaswa na madhambi yake kama vile moto unavyotakasa chuma. (Al-Bukhari).

*(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)*